

# Aina nyingi za UNYANYASAJI WA NYUMBANI



**Unyanyasaji wa Nyumbani unaweza kutokea katika njia mbalimbali tofauti. Ikiwa unajisikia kulazimishwa kufanya kitu, kuumizwa, au kuogopa nyumbani, ni muhimu kupata msaada.**

## UNYANYASAJI WA KIPESA

Ikiwa mtu anatumia pesa kukulazimisha kitu au kukuumiza. Inaweza kuonekana kama - kuzuia ufikiaji wako wa pesa, kukataza ufanye kazi au kuchukua mapato yako, au kulazimisha upate mkopo, rehani au mpango wa simu.

## UNYANYASAJI WA KISAIKOLOJIA

Ikiwa mtu anasema au kufanya mambo ya kukufanya uhisi hofu au mbaya juu yako mwenyewe. Inaweza kuonekana kama - kukutisha kukuumiza au kuumiza watoto, kukuita matusi, kuogopesha kwa kuendesha gari kwa hatari au kuharibu mali.

## UNYANYASAJI WA KIJAMII

Ikiwa mtu anajaribu kukukatisha na marafiki yako na familia. Inaweza kuonekana kama - kukukataza kuwaona marafiki au familia, kupunguza mawasiliano nao, au kuzuia matumizi yako ya gari au simu kutembelea/kuongea nao.

## UNYANYASAJI WA KIROHO

Ikiwa mtu anatumia imani za kiroho au kidini kukuumiza, kuogopesha au kukudhibiti. Inaweza kuonekana kama - kukuzuia usifanye mambo unayoamini, na kulazimisha ushiriki katika shughuli za kidini, au kutumia mafundisho ya dini kukufanya ubaki kwenye uhusiano au kukubali unyanyasaji au matumizi mabaya.

## UNYANYASAJI WA KIZAZI

Ikiwa mtu hukuzuia kufanya maamuzi yako kuhusu kama kupata watoto au la. Inaweza kuonekana kama - kulazimisha/kushinikiza wewe kuwa mjamzito au kuondoa mimba, kudhibiti kama unatumia au kutotumia dawa za mpango wa uzazi, au kuzuia ufikiaji wako kwa huduma za afya ya kingono.

**PATA USAIDIZI  
PATA MSAADA  
PATA USHAURI**

**POLISI - 131 444  
1800RESPECT - 1800 737 732  
HUDUMA YA KISHERIA YA KITAMADUNI MBALIMBALI -  
0401 963 582**

**WSCLC**  
WESTERN SYDNEY  
COMMUNITY  
LEGAL CENTRE

# Aina nyingi za UNYANYASAJI WA NYUMBANI



**Unyanyasaji wa Nyumbani unaweza kutokea katika njia mbalimbali tofauti. Ikiwa unajisikia kulazimishwa kufanya kitu, kuumizwa, au kuogopa nyumbani, ni muhimu kupata msaada.**

## UNYANYASAJI WA PICHA

Ikiwa mtu anasambaza au kutisha kusambaza picha zako za kibinafsi au za siri. Inaweza kuonekana kama - kusambaza au kutisha kusambaza picha za siri kwenye mitandao ya kijamii, kutisha kutuma picha za siri kwa marafiki na familia, au kuweka picha yako kwenye picha au video zisizofaa.

## KUWINDA NA KUOGOFYA

Ikiwa mtu anakunyanyasa kila mara kwa mawasiliano au umakini usiotakikana. Inaweza kuonekana kama - kupiga simu au kutuma maandishi kwako kila mara, kukufuata kwenda au kutoka nyumbani au kazini, au kufuatilia kwako bila idhini yako.

## UNYANYASAJI WA KIMWILI

Ikiwa mtu anasababisha madhara ya kimwili kwa makusudi. Inaweza kuonekana kama - kupiga, kupiga kofi au kupiga teke kwako, kutumia vitu kukuumiza, au kutemea mate kwako.

## UNYANYASAJI WA KINGONO

Ikiwa mtu anakulazimisha kufanya ngono bila idhini yako, hata kama umeoa au kuolewa. Inaweza kuonekana kama - kukugusa kingono, kulazimisha uguse mtu mwingine kingono, au kujamiana kwa kuingiza kichezeo, kidole au uume mdomoni mwako, mkundu au uke bila idhini yako.

## UNYANYASAJI WA WAZEE

Ikiwa mtu anapuuza mahitaji yako ya muhimu au kukusababishia madhara au dhiki. Inaweza kuonekana kama - kukuacha katika nguo zenye kichafu, kukuumiza kimwili, kusababisha hisia za aibu na unyonge, kukulazimisha kubadilisha wosia yako au kuweka saini kwenye hati, au kutumia pesa yako bila idhini yako.

**PATA USAIDIZI  
PATA MSAADA  
PATA USHAURI**

**POLISI - 131 444  
1800RESPECT - 1800 737 732  
HUDUMA YA KISHERIA YA KITAMADUNI MBALIMBALI -  
0401 963 582**

